

Kituo cha Msaada wa Majanga katika University City, Missouri Kitafungwa Wiki Ijayo

Release Date: Oktoba 26, 2022

Kituo cha Msaada wa Majanga katika University City kitafungwa kabisa Jumatano, Novemba 2 saa kumi na moja jioni (5pm)

Centennial Commons (Recreation Center)

7210 Olive Blvd.

University City, MO 63130

Kituo kimoja cha Msaada wa Majanga kitabakia wazi ili kuwasaidia waathiriwa walioathiriwa moja kwa moja na mafuriko ya Julai 25-28 na dhoruba kali:

Chuo cha Ranken Technical

Kituo cha Mary Ann Lee Technology

1313 N. Newstead Ave.

St. Louis, MO 63113

(Karibu na Kona ya Newstead na Page)

Isipokuwa ibainishwe vinginevyo, masaa za kituo cha msaada ni:

Jumatatu – Ijumaa, saa mbili asubuhi (8 a.m.)– saa kumi na mbili jioni (6 p.m.)

Jumamosi, saa mbili asubuhi (8 a.m.) – saa kumi na moja jioni (5 p.m.)

Inafungwa Jumapili



FEMA

Page 1 of 2

Katika vituo vya msaada, wataalamu kutoka FEMA na Usimamizi wa Biashara Ndogo ya Marekani wanatoa maelezo kuhusu huduma zinazopatikana, wakifafanua programu za usaidizi na kuwasaidia walionusurika kukamilisha au kuangalia hali ya maombi yao.

- Tuma ombi kwa FEMA mtandaoni kupitia [DisasterAssistance.gov](https://www.DisasterAssistance.gov) au piga simu kwa 800-621-FEMA (3362).
- Iwapo unahitaji usaidizi kutuma ombi, FEMA inaweza kukusaidia katika Kituo cha Msaada wa Majanga.
- Hakuna miadi inahitajika kutembelea Kituo cha Msaada wa Majanga. Wanaokuja bila miadi wanakaribishwa.
- Watu walioathiriwa moja kwa moja na mafuriko katika Jiji la St. Louis, Kaunti ya St. Louis na Kaunti ya St. Charles wanaweza kutembelea kituo chochote cha msaada kupata usaidizi wa ana kwa ana.

Kikumbusha: Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ya FEMA ni Novemba 7.

Kwa masasisho, tufuate kwenye Twitter [@MOSEMA](https://twitter.com/MOSEMA) na [@FEMARegion7](https://twitter.com/FEMARegion7).

Pata habari mpya kwa [Recovery.MO.gov](https://www.Recovery.MO.gov) na [FEMA.gov/disaster/4665](https://www.FEMA.gov/disaster/4665).

Usaidizi wa majanga unapatikana bila kuzingatia rangi, dini, utaifa, jinsia, umri, ulemavu, ujuzi wa Kiingereza au hali ya kiuchumi.



FEMA

Page 2 of 2